# LEARNING BY EAR

## “Mihadarati na vileo – Poromoko la jamii”

## Epsisode 7: “Athari za mihadarati”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**PROOFREADER: Charlotte Collins**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: BERI INTERROGATES PUYANGA AT THE POLICE STATION**

- **Beri (f, 45)**
- **Puyanga (m, 50)**

**SCENE TWO: AT HON. KIZITO'S MANSION**

- **Inspekta Tino (m, 40)**
- **Bamju (m, 40)**

**SCENE THREE: CHUNGA SANA, MAIN STREET**

- **Bi. Chacha (f, 45)**
- **Chambo (m, 30)**
- **Zula (m, 18)**
- **Okosho (m, 18)**
- **Peter (m, 18-40)**

- **Jabali (m, 18)**
- **4-5 Mixed voices (m/f)**

**<u>SCENE FOUR: AT THE POLICE STATION</u>**

- **Beri (f, 45)**
- **Waziri Kafegi (m, 55)**

**<u>SCENE FIVE: CHUNGA SANA, MAIN STREET</u>**

- **Bi. Chacha (f, 45)**
- **Chambo (m, 30)**
- **Zula (m, 18)**
- **Peter (m, 18-40)**
- **Jabali (m, 18)**
- **4-5 Mixed voices (m/f)**

**Msimulizi (m/f)**

**INTRO:**

Hujambo na karibu tena katika kipindi cha Noa bongo! Jenga maisha yako. Hiki ni kipindi cha saba katika hadithi hii inayoangazia ubadirifu wa mihadarati na vileo. Katika kipindi kilichopita, Beri aligundua kwamba bishara ya madawa ya kulevya inafanywa na watu wa ngazi za juu. Yaonekana mbunge wa eneo la Chunga Sana, Mheshimiwa Kizito pia yumo ndani. Okosho na Zula bado wanatafuta jinsi ya kujipatia madawa hayo ya kulevya, wakati Chambo na Jabali wako kwenye jumba la kurekebisha tabia waloathiriwa na madawa. Kipindi cha leo kinaitwa **“Athari za mihadarati”.** Na tunaanzia pale Beri akimhoji mumewe Puyanga aliyemkamata kwa kufanya biashara ya mihadarati.

**SCENE ONE: BERI INTERROGATES PUYANGA AT THE POLICE STATION**

1. **SFX: BUNCH OF KEYS OPENING AN IRON DOOR**

| | | |
|---|---|---|
| 2. | **BERI:** | Nani mwengine anayehusika na madawa haya ya kulevya, Puyanga? |
| 3. | **PUYANGA:** | Hata heshima huna, Beri? Mimi ni mumeo! Mabibi husalimia waume wao kwanza kabla ya kuzungumza -- |
| 4. | **BERI:** | **(cuts him short)** Usinipotezee muda, Puyanga. Nilijitahidi kufanya kila nilichoweza kuwa mke mzuri kwako. Wewe ni nini ulifanya kizuri kama mume wangu? Hakuna! Badala yake uliamuwa kuwa jangili. Kwa hiyo hapa ndani huna tofauti na mahabusu wengine, niambie ni nani mwengine mbali na Kizito? |

**5. PUYANGA:** **(shocked)** Kwani.. ulijuwaje? Beri, tafadhali usimuingize mheshimiwa Kizito kwa haya.. ninakurai…...

**6. BERI:** Kwanini? Siku za kuogopa watu wenye viti vikubwa serikalini zimekwisha, hawatafanya tena ugaidi tukiwatazama! Najua Kizito yuko ng’ambo kwa sasa , lakini nishamtuma Inspekta Tino nyumbani kwake. Na unajuwa ni nani anayekutana naye? Bamju! Anaamini umemtumia ujumbe mfupi huko akachukuwe madawa ya kulevya. Yote kupitia simu yako .

**7. PUYANGA:** Sawa, Beri. Nishakubali kuwa wewe ni askari bora. Utapewa madaraka mengine kama unataka. Lakini usifanye kosa hilo. Litawatia tope wakubwa wengi.

**8. BERI:** **(furious)** Kwa hiyo wataka kuendelea kusambaza mihadarati na vileo huku ukifanya wananchi wawe waathiriwa? Ukiwavunjia nyumba zao? Ukiongeza uhalifu, watoto wakiacha shule, magonjwa yakizidi na mauti kabla ya siku zao ili hali tunaweza kusitisha haya?

**9. PUYANGA:** Sawa. Mwataka ngapi?

**10. BERI:** Ngapi?

**11. PUYANGA:** Munataka pesa ngapi wewe na Tino? Najua mulipata pesa kwenye bidhaa zangu. Niambie munataka pesa ngapi na nitawapatia.

**12. BERI:** Kosa la pili hilo. Kujaribu kumuhonga afisa wa polisi. La, nashukuru, Puyanga. Ingawa mshahara wangu ni duni, lakini ni halali. Utakaa hapa usubiri kuhukumiwa.

**13. SFX: IRON DOOR BEING CLOSED AND LOCKED**

**14. PUYANGA:** **(shouting from inside)** na haki zangu je! Ala! Nahitaji kumpigia simu wakili wangu. Beri, simu moja tu. Tafadhali. Najuwa ninaruhusiwa simu moja.

**15. SFX: IRON DOOR BEING UNLOCKED AND OPENED**

**16. BERI:** Shika. Tumia simu yangu. Una dakika tatu, niko ofisini.

**17. MSIMULIZI:** Puyanga alijuwa wazi kuwa dakika tatu alizopewa ndizo aidha zingempa uhuru wake au kumtia jela kifungo cha maisha. Alichukuwa simu ya Beri na kupiga. Kisha akatabasamu, akafuta namba aloipiga kwa simu ya Beri na kumregeshea. Simu hii itaathiri nini katika kesi hii? Sio mbali tutayajuwa yote. Lakini kwa sasa, tutazame patashika ya Inspekta Tino akimsubiri Bamju afike nyumbani kwa mheshimiwa Kizito.

**<u>SCENE TWO: OUTSIDE HON. KIZITO'S MANSION</u>**

**18. SFX: FRONT DOOR BEING CLOSED FROM INSIDE**

**19. INSP. TINO:** Bamju, Mikono juu! Uko chini ya ulinzi!

**20. BAMJU:** **(taken by surprise)** Aah Hapana! Ni wewe tena, Inspekta Tino!

**21. INSP. TINO:** Umefika ukingoni, Bamju. Angusha mzigo.

**22. BAMJU:** Sawa, huu hapa….

**23. SFX: HEAVY BAG DROPPED + RUNNING FOOTSTEPS**

**24. INSP. TINO:** Wewe! Bamju, Simama!

**25. SFX: RUNNING FOOTSTEPS**

**26. INSP. TINO:** **(frustrated and out of breath)** Hapana! Ameniponyoka tena. Sikudhani anaweza kutoroka mbio namna hii. Hawa majangili wanafaa kubadilisha ajira zao wawe wakimbiaji! Eish! Lakini haidhuru nimeshika mzigo – bila shaka dawa za kulevya zimo ndani.

**27. MSIMULIZI:** Bamju alitimua mbio za swara kuona simba. Hakutaka kushikwa tena mara ya pili na Inspekta Tino. Kule mjini Chunga Sana, bado kuna patashika nyingine karibu kuanza, wahusika wakuu wakiwa Okosho, Zula na mwananke fulani.

**SCENE THREE: CHUNGA SANA, MAIN STREET**

**28. SFX: TYPICAL MAIN STREET AMBIENCE**

**29. ZULA:** **(worried)** Okosho, Una hakika na haya? Sijawahi kufanya jambo kama hili…….

**30. OKOSHO:** Zula, unataka kuzimuwa hutaki?

**31. ZULA:** Nina hamu kubwa, mameni… nasikia kama nitakuwa kichaa.

**32. OKOSHO:** Basi fanya ninavyokueleza. Kumbuka, nitakaponyakua wewe pia toka mbio. **(noticing something)** Aha, Yule mama pale anatoka kuchomoa bunda kwenye ATM.

**33. ZULA:** Habari, shangazi. Tafadhali nisaidie na kitu kidogo. Sijakula tangu jana.

**34. BI. CHACHA:** La. Samahani, sina pesa. **(hesitant)** Zula – ni wewe?

**35. ZULA:** **(shocked)** Bi. Chacha!

**36. SFX: A QUICK ROUGH SCUFFLE (studio)**

**37. BI. CHACHA:** **( Screams )** Wuuuui! Nisaideini! Wezi!!!! Kipochi changu!!!!!, wuuui!

**38. MIXED VOICES:** **(Shouts of "Mwizi! Mwizi!" fill the air from a mixed crowd)**

**39. PETER:** **(panting and trying to catch his breath)** Huyu - tume… tumemshika mmoja wao. Mwenye mkoba wako nasikitika ametoweka lakini huyu unaweza kumtambuwa?

**40. SFX: MURMURS AND COMPLAINTS FROM CROWD (studio)**

**41. ZULA:** **(begging))** Nisamehe, Bi. Chacha. Si mimi… naapa, mimi sijakuibia.

**42. BI. CHACHA:** Huyu alikuwa mwanafunzi wangu. Sikujua amekuwa mwizi wa mifuko….

**43. (Shouts of "Achomwe! Mvishe tairi!" fill the air from a mixed crowd)**

**44. PETER:** **(angrily)** Hawa mateja wametuchosha sasa. Ni lazima tupeane funzo kupitia kwenu kwa wale mateja wenzenu wanaotuibia kwa ajili ya uraibu wenu.

**45. ZULA:** Tafadhali musiniue...Nawaomba.. Nisameheeni

**46. SFX: SLAPS, BEATINGS, PEOPLE SPITTING (studio)**

**47. BI. CHACHA:** **(AKIJAARIBU KUINGILIA KATI)** Hebu, wacheni! Musichukuwe sheria mikononi!

**48. ZULA:** **(continous cries of agony)** Waah!... Uuuuh!... Arrrgh!..

**49. MSIMULIZI:** Kwa bahati mbaya au nzuri Chambo na Jabali walikua wanapita upande wa pili wa barabara

**50. SFX: STREET AMBIENCE**

**51. JABALI:** Chambo, unauona ule umati? Nikama ambae kuna mtu anapigwa. Hebu twende tutazame?

**52. CHAMBO:** Jabali, tuna kazi ya kufanya.Tayari tumeshachelewa. Kama unataka kushuhudia, wewe nenda tutaonana baadae..

**53. JABALI:** **(calls out hurriedly, already on his way over)** Sitakawia… **(Pause, STREET AMBIENCE GETS LOUDER)** Hebu, tafadhali kidogo, naomba kupita? Asante… asante sana...

54. **MSIMULIZI:** Huku Jabali akipenya umati ili afike kushuhudia, hakujuwa yaliokuwa mbele yake, katika kituo cha polisi Inspekta Tino na kamishna Beri walikuwa washamaliza kupeana taarifa ya mihadarati iliyopatikana nyumbani kwa muheshimiwa Kizito kwa wanahabari. Wakipongezana mara simu ya Beri ikaita.

**SCENE FOUR: AT THE POLICE STATION**

55. **SFX: MOBILE PHONE RINGING**

56. **BERI:** **(curious)** Hmm… Mbona anayepiga ameficha jina na namba yake? **(Answers phone)** Halo? Kamishna Beri.

57. **WAZIRI KAFEGI: (over the phone)** Wewe na Inspekta Tino kuanzia dakika hii mumehamishwa kutoka kituo hicho!

58. **BERI:** **(shocked)** Mimi si kutaniwa? Wewe ni nani?

59. **WAZIRI KAFEGI: (over the phone)** Kamishna Beri. Mimi ni waziri wa mambo ya humu nchini, Mheshimiwa Kafegi.

60. **BERI:** **(even more shocked)** Waziri Kafegi? Samahani mheshimiwa – sijui kama unafahamu lakini tuna kesi kubwa inayohusu madawa ya kulevya. Tumeshika kiasi kikubwa cha heroini.

61. **WAZIRI KAFEGI:** Ndio kiini cha kuwahamisha. Kesi hii imevutia askari wa kimataifa yani Interpol.

**62. BERI:** Lakini… mkubwa, nikifikiri ni mkuu wa polisi ndiye mwenye mamlaka ya kuhamisha askari polisi.

**63. WAZIRI KAFEGI:** **(getting angry)** Mkuu wa polisi anaripoti kwangu! Hii kesi ni kubwa sana na itakushinda. Wewe na inspekta wako nataka mufunge virago upesi, muna saa moja pekee. Kwaheri.

**64. SFX: BEEP SOUND AS WHEN MOBILE PHONE CALL IS ENDED**

**65. BERI:** Saa moja?! Haraka ni ya nini? Na kwanini hivi sasa? Kwani waziri wa mambo ya ndani pia anahusika na sakata hili?!

**66. MSIMULIZI:** Hiyo simu ilimpa mawazo mengi sana Beri – lakini alijuwa hakuwa na budi, ni lazima afikirie suluhu ya haraka. Hivi sasa Jabali alikuwa ameutawanya umati na kufika mbele, hapo akamuona rafikiye Zula akipigwa na umati. Jabali akaamuwa kutenda hatotizama tu.

**SCENE FIVE: CHUNGA SANA, MAIN STREET**

**67. SFX: SHOUTS AND NOISES FROM AN ANGRY CROWD (studio)**

| | | |
|---|---|---|
| **68.** | **JABALI:** | **(pleading)** La! Tafadhalini ngojeni! Wacheni kumpiga – namjuwa huyu kijana si mwizi. |
| **69.** | **PETER:** | Wewe! Pia wewe ni mmoja wao? Wewe pia tutakuvisha “tairi” tukuwashe moto! |
| **70.** | **ZULA:** | **(still in tremendous pain)** Ah Jab…ali… Pole, mameni. Tu.. limuibia Bi. Chacha... mkoba wake, tulihitaji pesa za haraka tununue mihadarati, si unajuwa. Na... Okosho ametoroka na mkoba huo. Arrrgh! Mwili wote waniuma... |
| **71.** | **JABALI:** | Bi. Chacha! Mungu wangu… Tafadhalini, nawaomba nyoteni, msameheni Zula. Nawaapia, hii ni mara yake ya kwanza kuiba – mumemsikia wenyewe kuwa aliiba ili apate pesa za kununulia mihadarati. Huyu ni mgonjwa. |
| **72.** | **PETER:** | Mgonjwa? Mgonjwa wapi? Huyu ameathiriwa na madawa ya kulevya. |
| **73.** | **JABALI:** | Kuathirika ni ugonjwa. Hata mimi nimejifunza leo. Rafiki yangu Zula anahitaji matibabu.Tafadhalini muhurumieni. |

**74. BI. CHACHA:** Naunga mkono. Lakini mkoba wangu una shilingi 5,000 ndani yake. Nitamsamehe kama zitarudi taslimu hizo pesa na stakabadhi zilizomo humo ndani ziwe timamu.

**75. JABALI:** Utapata kila kitu chako kamilifu Bi. Chacha. Nakuahidi. Na nyinyi wengine mwasemaje? Sikilizeni – najuwa kuwa majumbani mwetu muna watu ambao wanapambana na athari za mihadarati – inaweza kuwa sigara, bangi, mirungi, au pombe, au hata dawa nyenginezo kama za maumivu…Labda hata wengine wenu muko hapa, hatuna tofauti na rafiki yangu Zula. Mumempiga vyakutosha. Ashatubu. Tafadhalini – mpeni nafasi abadilishe maisha yake.

**76. SFX: MURMURS FROM THE CROWD BECOME SOFTER AND CALMER (studio)**

**<u>OUTRO:</u>**

Huku Jabali akisihi umati na kushika kichwa cha Zula kilichokuwa kikivuja damu kwa pigo alopata, tunatamatisha kipindi cha saba cha tamthilia hii kwa jina **“Poromoko la jamii”,** kuhusu mihadarati na vileo. Je Zula amefika chini kabisa? Yuko tayari kubadili maisha yake? Beri atafanyaje baada ya kupata amri ya uhamisho wa ghafla? Usikose kipindi kijacho, kwani majibu utapata hapo. Kusikiliza tena hiki kipindi au vingine vilotangulia, tembelea www.dw.de/lbe.Hadi wakati mwengine. Kwaheri.